TANGAZO LA SERIKALI NA. 783 la tarehe 30/8/2024

SHERIA YA UDHIBITI WA SILAHA NA RISASI,
SURA YA 223

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 64)*

NOTISI YA MSAMAHA KWA WAMILIKI WA SILAHA KINYUME CHA SHERIA, YA MWAKA 2024

KWA KUWA, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizosaini na kuridhia mikataba, itifaki, maazimio na makubaliano mbalimbali kuhusu kuzuia silaha ndogo na nyepesi ikiwa ni pamoja na Makubaliano ya Umoja wa Mataifa yaliyofanyika mwezi Julai 2018;

KWA KUWA, Nchi wanachama wa Umoja wa Afrika zilifikia maazimio juu ya Udhibiti wa silaha haramu katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika uliofanyika tarehe 03 hadi 04 Julai,2017 jijini Addis Ababa - Ethiopia na kuazimia Mwezi Septemba kuwa Mwezi wa usalimishaji wa silaha haramu kwa hiari sambamba na kutoa msamaha kwa wahusika kutoshitakiwa iwapo watasalimisha silaha hizo kwa hiari katika muda uliopangwa;

NA KWA KUTAMBUA KUWA, uzagaaji wa silaha haramu duniani umekuwa ukisababisha uvunjifu wa amani, ukosefu wa usalama, hofu kwa watu, vifo na majeruhi;

NA KWA KUWA, kifungu cha 64 cha Sheria ya Udhibiti wa Silaha na Risasi, Sura ya 223 kinampa Waziri mamlaka ya kutoa msamaha wa kutoshitakiwa kwa watu wanaomiliki silaha kinyume cha Sheria kwa madhumuni ya kulinda amani na kuwawezesha watu hao kusalimisha silaha wanazomiliki kinyume cha Sheria;

HIVYO BASI, Mimi HAMAD M.Y. MASAUNI, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, katika kutekeleza mamlaka niliyopewa chini ya kifungu cha 64 cha Sheria ya Udhibiti wa Silaha na Risasi, ninatoa Notisi kama

ifuatavyo:

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Msamaha kwa Wamiliki wa Silaha Kinyume cha Sheria ya Mwaka 2024.

Usalimishaji wa silaha haramu

2. Kwa kuzingatia masharti ya aya ya 3 ya Notisi hii, mtu anayemiliki silaha kinyume cha Sheria atakayesalimisha silaha hiyo atasamehewa na kutoshitakiwa kwa umiliki wa silaha kinyume cha Sheria.

Masharti ya msamaha

3.-(1) Mtu yeyote hatashitakiwa kwa umiliki wa silaha kinyume cha msamaha iwapo atasalimisha silaha kwa hiari kwa kuzingatia utaratibu ulioainishwa katika Notisi hii.

(2) Utaratibu wa usalimishaji wa silaha haramu kwa hiari utafanyika kuanzia tarehe 1 Septemba, 2024 hadi 31 Oktoba, 2024.

(3) Silaha haramu zitasalimishwa katika kituo chochote cha polisi nchini, ofisi ya serikali ya mtaa, kwa mtendaji kata au Shehia kuanzia muda wa saa mbili asubuhi hadi saa kumi jioni.

Ukomo wa msamaha

4.-(1) Msamaha utakaotolewa kwa mujibu wa Notisi hii utakuwa ni kwa mwezi wa Septemba na Oktoba.

(2) Mtu yeyote atakayesalimisha silaha haramu nje ya muda ulioainishwa katika Notisi hii atachukuliwa hatua za kisheria.

Dodoma,
28 Agosti, 2024

HAMAD M.Y MASAUNI
*Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi*